**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukur Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena katika chombo hiki muhimu tukiwa wazima wa afya ili tuweze kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba ya kuwatumikia wananchi katika Mkutano huu wa Bajeti kwa kujadili, kushauri na hatimae kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo Biashara na Utalii, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee kabisa naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii ambao wamejitoa kwa hali na mali kwa lengo la kuisaidia Serikali kutimiza malengo yake kwa wananchi kwa michango yao mizuri pamoja na uchambuzi wa kina walioufanya kuhusiana na bajeti hii. Michango na maoni yao imesaidia sana katika uandaaji wa hotuba hii pamoja na kuisaidia Wizara kurekebisha pale ambapo Wajumbe walielekeza.

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima kubwa kabisa naomba niwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ameir | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Azza Januari Joseph | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ali Abdulgulam Hussein | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Said Saleh Salim | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Aziza Waziri Kheir | Katibu |
| 9. | Ndg. Mwaka Mwinyi Waziri | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,** Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizojaaliwa kuwa na idadi kubwa ya vivutio vya utalii kuanzia kwenye maeneo ya kihistoria mapango na misitu ya asili ambayo huwavutia watalii kwa kiasi kikubwa. Katika kuiimarisha sekta ya Utalii nchini, Serikali ya awamu ya nane imeahidi kuendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuikuza na kuiendeleza sekta hii pamoja na kuwepo kwa changamoto kubwa ya maradhi ya Corona ambayo kwa kiasi kikubwa imerudisha nyuma maendeleo ya sekta utalii.

**Mheshimiwa Spika**, katika uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr Hussein Ali Mwinyi alisema kuwa kwa vile sekta ya utalii ndio muhimili mkuu wa uchumi wa nchi yetu, atahakikisha Serikali yake inashirikiana na sekta binafsi kuitangaza Zanzibar katika masoko ya asili na masoko mapya pamoja na kuendelea na ujenzi wa hoteli za daraja la juu na miundombinu muhimu yote itakayonyanyua utalii wetu hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha malengo ya Serikali yanafikiwa, Kamati ya Kilimo Biashara na Utalii inaamini kuwa malengo hayo yatafanikiwa endapo tu fedha zilizotengwa ndani ya bajeti tuliyoipitisha zitapatikana kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu ilianza kupitia bajeti ya Wizara hii kwa kuangalia mapato ya Wizara na taasisi zake mbali mbali ambazo zinakusanya mapato. kwa kiasi kikubwa Kamati iliridhika ingawa kulikua na baadhi ya maeneo Kamati ilitoa maoni yake kuhusiano na ukusanyaji wa mapato hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipewa mchanganuo wa mapato ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ambapo katika mchanganuo huo, haikufafanuliwa kwa maelezo ya kina kwa kila Idara ambayo inakusanya mapato ilikusanya kiasi gani kwa mwaka na kupelekea masuali mengi ya Wajumbe kuhusiana na jambo hilo. Kutokana na hali hiyo,

Kamati yangu imeishauri Wizara kila inapotoa mchanganuo wa mapato, kila idara ifanyiwe mchanganuo wake ili ijulikane kila idara ilifanya makusanyo kwa kiasi gani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia iliangalia mapato Katika Kamisheni ya Utalii yanayotokana na vibali na stika ambapo ilishauri mapato hayo yachanganywe katika stika ili kuepuka rushwa. Aidha, Kamati ilishauri mapato hayo yakusanywe kwa kutumia mfumo maalum na badala ya kuwa na mapato katika stika,vibali na leseni tubakiwe na makusanyo kwa njia mbili tu yaani stika na leseni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inatoa ushauri kutokana na ukweli tunaoupata katika msemo wa kiswahili usemao ***'Mtu yeyote asiyetunza pato lake dogo, hawezi kuwa tajiri'***, hayo ni maneno ya msanii nguli barani Afrika bwana **Shaaban Robert** aliyoyasema katika Riwaya yake ya ***'Kusadikika'.*** Sisi Kamati tunaamini kuwa, pato letu ni dogo lakini pamoja na udogo wake ni vyema tukakusanya kwa utaratibu maalum ili tija yake iweze kuonekana.

**Mheshimiwa Spika,** katika ukusanyaji wa mapato kwa upande wa Wizara, Kamati inashauri mapato yote yakusanywe kwa pamoja kupitia kibali kimoja tu katika Idara ya Makumbusho ya Kale kwa kuweka utaratibu maalum. Aidha katika uchambuzi wa mapato kwa Mamlaka ya Mji Mkongwe Kamati ilibaini kupandishwa kwa makadirio kwa Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa mwaka 2021/2022 na kuekewa shilingi milioni 100 kutoka shilingi milioni 45. Kamati ilishanganzwa na hali hii kutokana na uhalisia kwamba vianzio vya mapato vya Mamlaka ni vile vile havijaongezeka lakini mapato yametakiwa kuongezeka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imeshangazwa sana na hali hiyo na inaishauri Wizara ya Fedha inapopanga makisio ya mapato waangalie na hali halisi ilivyo na sio kuziongezea mzigo Idara/ Taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ilipitisha bajeti ya Wizara hii kwa kutoa maelekezo na ushauri kidogo ambao Wizara iliahidi kuufanyia kazi ili malengo ya mwaka huu wa kibajeti yaweze kukamilika kwa wakati. Kwa mwaka 2021/2022 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imepanga kutekeleza Programu kuu tano kama zifuatazo:-

i) Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii;

ii) Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe;

iii) Programu ya Utawala na Uendeshaji;

iv) Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii; na

v) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Kamisheni ya Utalii.

**PROGRAMU YA KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII**

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii utekelezaji wake unahitaji fedha nyingi ingawa bajeti yetu ni finyu ukilinganisha na majukumu ya utekelezaji yaliyowekwa. Hata hivyo, tunaamini kuwa hicho hicho kidogo kilichopangwa kikipatikana kwa wakati kitaweza kufanikisha lengo lililokusudiwa kwa kiasi fulani.

**Mheshimiwa Spika**, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi iliweka malengo katika sekta ya utalii ya kuongeza idadi ya wageni wanaoitembelea Zanzibar kutoka **538,264** mwaka 2019 hadi kufikia wageni **850,000** mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,** malengo hayo yatafanikiwa endapo tutajipanga katika suala zima la kuviimarisha vivutio vyetu vya utalii ambavyo vitawafanya wageni wavutike na wahamasike kuja kutembelea nchi yetu kwa wingi. Kamati inashauri kulifanyia matengenezo makubwa jengo la makubusho la Baytul Amin ambalo limechakaa kwa kiasi kikubwa. Ukarabati wa jengo hili utasaidia kuongezeka kwa wageni watakaotembelea jengo hilo ambalo lina historia kubwa hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa programu hii, Kamati inaamini kuwa endapo wananchi wanaotembelea katika Makumbusho ya kale na kutumia nyaraka zilizopo katika makumbusho hayo watatakiwa kulipa chochote kama tozo itasaidia kuinua pato letu linalotokana na Utalii na kupelekea nchi yetu kunufaika kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, dhana ya Utalii kwa wote iliyoanzishwa na awamu iliyopita ilikua na lengo la kuhakikisha kila mwananchi ananufaika na sekta ya utalii moja kwa moja kwa kuwahamasisha wananchi kuwekeza katika sekta ya utalii. Lengo hili litafikiwa endapo tu Kamisheni ya Utalii na Idara nyengine husika zitapatiwa fedha za kutosha Kutimiza wajibu katika hili.

**Mheshmiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu hii ilipangiwa jumla ya shilingi **2,311,633,000** fedha ambazo zimeongezeka kidogo ukilinagnisha na bajeti iliyopita ambapo makadirio kwa mwaka 2020/2021 zilikuwa ni shilingi **2,277,784,000** fedha ambazo hazikupatikana zote katika utekelezaji wake.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii imelenga kuhifadhi, kuyaimarisha na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria yakiwemo ya Mji Mkongwe kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae. Lengo la Serikali kwa sasa ni kuona kuwa jamii imeelewa kwa kiasi kikubwa kuhusiana na suala la utalii kwa kulinda na kuimarisha tamaduni zetu pamoja na kuyathamini maeneo ya kale pamoja na kuendeleza historia na urithi wa Zanzibar ukiwemo Mji Mkongwe ambao umepata umaarufu duniani kote.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali pamoja na nia nzuri iliyonayo, lakini tukiangalia uhalisia katika utekelezaji wa bajeti iliyopita bado kuna juhudi kubwa zinahitaji kuchukuliwa ili tuweze kukamilisha mipango hiyo. Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii inapenda kuchukua nafasi hii kuelezea masikitiko yake kuhusiana na suala zima la kuanguka kwa jengo la ***'Bait Al Ajaib'*** pamoja na juhudi kubwa zilizochuliwa na Serikali katika suala hilo, na tunaipongeza Serikali na Rais wetu wa Zanzibar kwa kuchukua hatua za haraka katika suala hilo, lakini sisi kama Kamati tunasisitiza umuhimu wa kukamilika kwa ukarabati wa jengo lile ambalo linaingiza kipato kikubwa kwa taifa na linaingiza mapato mengi ambayo yanawasaidia wananchi wetu katika mambo mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 programu hii imekadiriwa jumla ya shilingi **6,115,154,000** ambazo zitatumika katika maeneo mbali mbali yalivyoelezwa na Wizara katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Hata nhivyo, Kamati inasisitiza kuwa kutokana na miradi mingi ya kimkakati kukwama utekelezaji wake katika bajeti iliyopita kutokana na sababu mbali mbali, tunaishauri Serikali kwa bajeti hii tunayoipitisha fedha zake zipatikane kwa wakati ili ile athari ya utekelezaji iweze kuonekana na wananchi wanufaike na matunda ya Utalii kutokana na juhudi zao za kuyalinda maeneo ya kihistoria.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia bajeti hii tunapenda kuishauri Serikali na Wizara kwa ujumla kupitia taasisi zake kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya suala zima la uhifadhi wa maeneo ya kihistoria. Katika ziara za Kamati katika baadhi ya maeneo, Kamati ilibaini changamoto ya baadhi ya wananchi kufanya uharibifu mkubwa wa maeneo ya kihistoria hasa wale wananchi wanaoishi karibu na maeneo hayo.

## PROGRAMU YA UTAWALA NA UENDESHAJI

**Mheshimiwa Spika**, programu hii inabeba mambo mengi ya msingi yakiwemo ya kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti mbalimbali pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii ina programu ndogo

tatu ambazo ni Utawala na uendeshaji katika sekta ya Utalii na Mambo ya Kale, kuratibu na kusimamia mipango mikuu ya Wizara na kuratibu na kusimamia utawala, uendeshaji na mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa programu hii unahitaji umakini na fedha za kutosha ili malengo yaliyopangwa yaweze kutimia kwa wakati. Kama tunavyojua rasilimali watu ni nyenzo muhimu sana ambapo mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi yanahitaji kutengenezwa ili kile kilichopangwa kiweze kufanikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokua inafanya ziara katika baadhi ya maeneo ilijionea changamoto mbali mbali ambazo zinahitaji utatuzi wa haraka ili malengo ya Wizara yaliyoapngwa yaweze kutimia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2021/2022programu hii imekadiriwa kutumia shilingi **2,447,061,000** fedha ambazo ni kidogo kutokana na malengo yaliyowekwa. Hata hivyo, tunashauri hichi hichi kidogo kilichopangwa kipatikane kwa wakati ili angalau hata kidogo tuweze kutekeleza kwa asilimia kubwa kabisa.

## KAMISHENI YA UTALII

**Mheshmiwa Spika**, Kamisheni ya Utalii ina jukumu la kuhamasisha utalii wa ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na wadau mbali mbali katika kuhakikisha kuwa dhana ya Utalii kwa wote inafikiwa na faida kwa wananchi inapatikana.

**Mheshimiwa Spika**, Kamisheni ya Utalii katika utekelezaji wa malengo yake ina programu kuu mbili ambazo ni Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Kamisheni ya Utalii.

## PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI WA UTALII

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la programu hii ni kuongeza tija kwa jamii pamoja na kuongeza idadi ya watalii na thamani yao izidi kuongezeka kwa kuwawekea mazingira mazuri yatakayowavutia na kuwahamasisha kuingia kwa wingi nchini.Programu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko ambayo ina jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi ili nchi yetu itambulike kuwa ni miongoni mwa vituo bora vya utalii duniani.

**Mheshimiwa Spika,** ikiwa programu hii imelenga pia kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusiana na huduma zinazopatikana katika sekta nzima ya Utalii, ni vyema idara ya masoko inapoandaa mikakati ya kuitangaza nchi yetu kwa kuandaa matamasha mbali mbali na maonehso ya kibiashara ikawashirikisha wananchi moja kwa moja ili wananchi

hao wazidi kuhamasika na kuitangaza nchi yetu katika maeneo ambayo pengine Kamisheni haikuyafikia.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuuendeleza Utalii, Kamati inasisitiza kuwa kuna umuhimu mkubwa kwa Wizara ya Utalii kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano katika suala zima la kuiendeleza na kuijenga upya miundombinu ya barabara nyingi zilizopo katika maeneo ya Utalii ambazo nyingi kwa sasa zimeharibika na baadhi hazipitiki kabisa. Kupitia bajeti hii tunaiomba Serikali ilitilie mkazo suala hili kwa kuzijenga barabara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kuna baadhi ya maeneo yana vivutio vingi vya utalii lakini maeneo hayo miundombinu yake haiko vizuri kama maeneo yaliyoko katika Wilaya ya Micheweni.

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio ya programu hii yataonekana kupitia ongezeko la idadi ya watalii wanaoingia nchini, hivyo ni vyema bajeti inapopangwa iangalie na shughuli mahususi zinazopangwa ili yale malengo yanayopangwa yaweze kukamilika. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi **595,510,000** fedha ambazo ni kidogo ukilinganisha na bajeti iliyopita ambapo makadirio kwa mwaka 2020/2021 yalikuwa ni shilingi **602,830,000**. Kutokana na hali hiyo tunashauri fedha za bajeti zinapopangwa yaangaliwe yale majukumu halisi yaliyopo na uzito wa sekta husika ulivyo ili yale yote yaliyoahidiwa na Serikali yaweze kukamilika kwa wakati.

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA KAMISHENI YA UTALII

**Mheshimiwa Spika**, programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu na mizuri katika sekta ya utalii pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Kamisheni ya Utalii.

**Mheshmiwa Spika,** mafunzo kwa watoa huduma wa sekta ya utalii ni muhimu hivyo, katika utekelezaji wa programu hii, Kamati inashauri watoa huduma wa sekta ya utalii wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara ili waweze kutimiza wajibu wao vizuri. Aidha tunashauri mafunzo hayo yatolewa kwa kuzingatia ukubwa wa majukumu na kuwashirikisha wafanyakazi wote wa Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika**, makadirio ya bajeti ya mwaka huu wa 2021/2022 kwa programu hii ni shilingi **1,447,390,000** fedha ambazo zimepungua kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na makadirio ya bajeti iliyopita ambapo makadirio yalikua ni jumla ya shilingi **3,512,470,000**. Kamati imesikitika na kiwango hiki cha fedha lakini hatuna budi kukubaliana na hali halisi kwa kujipanga kukitumia hicho hicho kidogo

kilichowasilishwa kwani waswahili wanasema ***'Hakuna sikio gumu duniani lisilosikia vinywa vingi vikisema kwa umoja'***. Hayo si maneno yangu bali ni ya Bwana **Shaaban Robert** aliyoyasema katika Riwaya yake mahiri ya ***'KUSADIKIKA'***.

**Mheshimiwa Spika**, naamini kuwa vinywa vya Wajumbe walio wengi humu ndani vikipaza sauti kuhusiana na ufinyu wa bajeti tulionao katika Idara mbali mbali za Serikali, basi naamini watumishi wa Umma watafanya kazi kwa bidii kutimiza wajibu wao, wananchi na wafanyabiashara wanaokwepa kulipa kodi watalipa kodi kwa wakati ili makusanyo yazidi kuimarika na kuwa mengi zaidi na hatimae Serikali itaweza kuongeza fedha kwa taasisi zetu hizi ili kazi tuliyoianza ya kulijenga taifa letu iweze kukamilika kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii pia kuihamasisha Kamisheni ya Utalii kuendelea na jukumu lake la msingi la kuutangaza utalii ndani na nje ya nchi kwa kubuni vyanzo vyengine vya mapato ambavyo vitakubalika kitaifa kwa lengo la kuongeza pato la taifa.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii katika Baraza lako tukufu, pia niwashukuru Wajumbe wako kwa utulivu wao waliouonesha wakati nawasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Nawaomba Wajumbe wako waichangie bajeti hii, wahoji na watoe mapendekezo yao pale panapohitajika na hatimaye kuipitisha baada ya kuafikiana kwa hoja mbali mbali watakazoziibua wakati wa mjadala.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

……………………………………..

**Azza Januari Joseph,**

**Makamo Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii,**

**Baraza la Wawakilishi,**

**<u>Zanzibar.</u>**